



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. FB.192/247/01/B/124

28 Mei, 2024

Kwa Taasisi Nunuzi Zote na Wadau wa Ununuzi wa Umma;

**YAH: MPANGO WA MAFUNZO YA MFUMO WA KIELEKTRONIKI
WA UNUNUZI WA UMMA (NeST) KWA MWEZI JUNI 2023.**

Tafadhali rejea kichwa cha habari hapo juu.

2. Serikali imetengeneza Mfumo mpya wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST), ambao umeanza kutumika kuanzia Mwezi Julai, 2023 ikiwa ni sambamba na Sheria Mpya Na. 10 ya 2023 ambayo itaanza kutumika mwezi Juni 2024 na Kanuni zake kuanza kutumika kuanzia tarehe 1 Julai 2024. Kwa mantiki hiyo, PPRA imeandaa Mpango wa Mafunzo kwa mwezi Juni, 2024, kwa ajili ya wadau wa ununuzi wa umma. Mafunzo haya yatafanyika katika Mikoa ya **Arusha, Mbeya, Mwanza, Dar es Salaam, Mtwara na Tabora** zilipo ofisi za kanda za Mamlaka.
3. Mafunzo ya kutumia mfumo yatatolewa kwa muda wa siku tano (5) kwa Taasisi Nunuzi na siku moja (1) kwa Wazabuni. Ada kwa kila mshiriki ni TZS 550,000.00; kutoka katika Taasisi Nunuzi na TZS 100,000.00, kwa kila Mzabuni.
4. Maafisa Masuuli wanahimizwa kuwatuma washiriki kutoka kwenye taasisi zao kwa kuchagua vituo na tarehe za mafunzo zinazoonekana kwenye Kalenda iliyoambatishwa. Washiriki watathibitisha ushiriki wao kwa kujiandikisha na kulipia ada ya Mafunzo PPRA kupitia tsms.ppra.go.tz.
5. Ninawashukuru kwa ushirikiano wenu.

Eliakim C. Maswi
MKURUGENZI MKUU

**KALENDA YA MAFUNZO YA MFUMO WA KIELEKTRONIKI WA UNUNUZI WA
UMMA (NeST) KWA MWEZI JUNI 2023**

Washiriki: AOs, TB Members, PMU, UD, LAs, LOs Taasisi Nunuzi

NA	TAREHE	KITUO	IDADI YA WASHIRIKI	GHARAMA (TSH)
1.	24 – 28 Juni, 2024	Arusha,	150	550,000
2.	24 – 28 Juni, 2024	Dar es Salaam	150	550,000
3.	24 – 28 Juni, 2024	Mbeya	150	550,000
4.	24 – 28 Juni, 2024	Mtwara	150	550,000
5.	24 – 28 Juni, 2024	Mwanza	150	550,000
6.	24 – 28 Juni, 2024	Tabora	150	550,000

Washiriki: Wazabuni

NA	TAREHE	KITUO	IDADI YA WASHIRIKI	GHARAMA (TSH)
1.	29 Juni, 2024	Arusha,	150	100,000
2.	29 Juni, 2024	Dar es Salaam	150	100,000
3.	29 Juni, 2024	Mbeya	150	100,000
4.	29 Juni, 2024	Mtwara	150	100,000
5.	29 Juni, 2024	Mwanza	150	100,000
6.	29 Juni, 2024	Tabora	150	100,000